

## Mradi wa kusaidia watoto wazinduliwa

■ Na Ashura Ally

**W**IZARA ya Kazi na Ajira ikishirikiana na Taasisi isiyo ya kiserikari ya Winrock International imezindua mradi ujulikanao kama Prosper ili kutokomeza utumikishwaji wa watoto katika mashamba ya tumbaku mkoani Tabora.

Akizindua mradi huo juzi, Waziri wa wizara hiyo, Gaudensia Kabaka alisema mradi huo utaanzia Wilaya za Urambo na Sikonge kwani sehemu hizo zimekuwa na mfumuko mkubwa wa watoto kutumikishwa katika mashamba hayo.

Waziri alisema lengo la mradi huo ni kuwalinda watoto walio na umri chini ya miaka mitano hadi 15 ili kuwaepusha na madhara yatoakanayo na kufanya kazi za aina hiyo.

Aliwataka wananchi kuwapa ushirikiano wasimamizi wa mradi huo badala ya kuwatenga ili wafanye kazi yao kwa ufanisi.

Makamu wa Rais wa mradi wa Prosper, Barbara Martellinalisema malengo yao si kupunguza tatizo hilo bali ni kulitokomeza kabisa bila kujali mtoto anayesaidiwa ni Mtanzania au la.